HOTUBA YA MHE. JOHN. P. MAGUFULI (MB) WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI KWENYE UZINDUZI WA BARAZA LA MWAKA LA WADAU WA SEKTA NDOGO YA NYAMA KATIKA UKUMBI WA HOTELI YA OASIS, MOROGORO, TAREHE 10/03/2008.

Ndugu Mwenyekiti wa Baraza,
Wawakilishi kutoka Taasisi za Serikali
Wawakilishi kutoka Taasisi zisizo za Kiserikali,
Ndugu Wafugaji, Wazalishaji wa Mifugo, na wadau wengine,
Ndugu Wataalam wa Mifugo,
Ndugu Wageni Waalikwa,
Mabibi na Mabwana.

Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru waandaaji wa mkutano huu kwa kunipa fursa hii ya kuzindua Baraza la Mwaka la Wadau wa Sekta Ndogo ya Nyama. Natoa pongezi hizi maalumu kwa sababu tangu niteuliwe na Mhe. Rais kuiongoza Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, sijapata nafasi ya kuongea na kundi kubwa la wadau kama ninyi hapa leo hii. Napenda pia kuwapongeza wajumbe wote wa Baraza hili kwa kuteuliwa kuwa wawakilishi katika Baraza hili muhimu kwa maendeleo ya Nyama nchini. Naamini Mikoa, Wilaya na Taasisi mbali mbali zilizowateua zina imani kubwa nanyi ya kuiendeleza sekta ya Mifugo na hususan zao la nyama.

Aidha napenda nichukue fursa hii kuwakaribisha wote kwenye mkutano huu wa kwanza wa Baraza unaofanyika katika Manispaa ya Morogoro, mjisikie huru kwa kipindi chote mtakachokuwa hapa. Mahudhurio yenu yanadhihirisha kukubali kwenu na kuelewa kuwa jukumu la kuendeleza sekta hii hapa nchini ni la wadau wote na ushiriki wenu ni muhimu katika kufikia lengo hilo.

Ndugu Mwenyekiti, nimeambiwa kwamba Baraza hili lina wajumbe wanaowakilisha wadau mbalimbali kutoka wilaya zote za Tanzania Bara, vyama vya kitaifa vya wadau, yaani wazalishaji, wasindikaji na wafanyabiashara, mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi mbali mbali. Nina imani kwamba ninyi mlioteuliwa mtawakilisha mawazo na michango ya wadau wengine wote.

Licha ya kwamba mtakuwepo hapa kwa siku mbili tu kujadili namna ambavyo Baraza hili litasimamia utekelezaji wa Sheria ya Nyama ya mwaka 2006, naamini mtaitumia siku hii vizuri kadri ya uwezo wenu. Baraza hili limeundwa kisheria ili kuindeleza sekta hii kibiashara na kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zinazozalisha zao la nyama kwa ubora na wingi katika Bara letu la Afrika na Ulimwenguni. Hivyo ni matarajio yangu kwamba endapo Baraza hili litatekeleza wajibu wake ipasavyo, tutaweza kutoa hamasa kwa wafugaji wetu kuzalisha kwa kuzingatia misingi ya kibiashara na hatimaye kuwakwamua wafugaji toka kwenye lindi la umaskini na kuongeza mchango wa sekta yetu katika pato la Taifa.

Ndugu Mwenyekiti, nafahamu mtapata nafasi ya kujadili mada muhimu zikiwemo ya ufafanuzi wa Sheria ya Nyama ya mwaka 2006, majukumu ya Baraza la Mwaka la Wadau, uzalishaji wa mifugo kibiashara na masoko ya mifugo ya nyama na mazao yake hapa nchini ambazo zimelenga kutoa hamasa itakayowawezesha kutekeleza taratibu za kuunda Bodi itakayosimamia shughuli nzima ya uzalishaji na biashara ya nyama hapa nchini.

Ndugu Mwenyekiti, Tanzania ina rasilimali ya eneo kubwa la malisho na idadi kubwa ya mifugo. Takwimu zinaonyesha kwamba kati ya hekta milioni 88.6 za ardhi iliyopo hapa nchini, hekta milioni 60 ni za malisho zinazoweza kutumika kwa ufugaji. Eneo hilo la malisho lina uwezo wa kulisha mifugo takriban ng'ombe wakubwa milioni ishirini. Takwimu pia zinaonyesha kuwa Tanzania ina Ng'ombe milioni 18.8, Mbuzi milioni 13.1, Kondoo milioni 3.6, Nguruwe milioni 1.37, Kuku wa kienyeji milioni 33 na wa kisasa milioni 20. Sehemu kubwa ya mifugo hii ni ya asili ambayo inaongezeka kwa kiasi cha asilimia mbili tu kwa mwaka. Pamoja na ukubwa wa rasilimali hii, Sekta ya mifugo inachangia kiasi cha asilimia **6.1** tu ya pato la Taifa, kiasi ambacho sote tunaamini tunaweza kukiongeza. Kama mtakumbuka Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 imetuagiza tuongeze mchango wa sekta ipasavyo na napenda kunukuu:

" a) Kujenga mazingira ya kuvutia uwekezaji katika viwanda vya kuongezea thamani mazao ya mifugo kama vile ukataji nyama, usindikaji wa maziwa, utengenezaji wa bidhaa za ngozi n.k.

b) Kuwashawishi Watanzania wale nyama na mayai na kunywa maziwa kwa wingi zaidi kwa ajili ya kujenga afya zao na kukuza soko la ndani la bidhaa hizo.
c) Kufufua na kujenga mabwawa na majosho mapya kwa ajili ya mifugo
d) Kuwaelimisha wafugaji umuhimu wa kuuza sehemu ya mifugo yao ili wajipatie mapato.
e) Kuwahimiza wafugaji kutekeleza Kanuni za ufugaji bora na kwa ujumla kuwawezesha kuingia katika ufugaji wa kisasa.
f) Kuhifadhi mazingira kwa kuzingatia ufugaji endelevu usioharibu mazingira, rasilimali muhimu kama ardhi na vyanzo vya maji kote nchini.
g) Kuendelea kukuza na kuendeleza masoko ya ndani ya mifugo na mazao yake.
h) Kuendeleza mikakati ya kukuza sekta ya mifugo kupitia ugani, tiba, kinga, usambazaji wa maji na uboreshaji wa malisho.
i) Kuimarisha vituo vya uzalishaji wa mbegu za ng'ombe na mifugo mingine na kuongeza ufanisi katika usambazaji wa mbegu hizo.
j) Kuendelea kutenga maeneo ya wafugaji kwa lengo la kupunguza migogoro baina ya wakulima na wafugaji.
k) Kuendelea kuhamasisha uimarishaji na uanzishaji wa vikundi vya ushirika wa wafugaji".

Mwisho wa kunukuu.

Ndugu Mwenyekiti, aidha, malengo ya Mkukuta na yale ya milenia (MDG) ya kupunguza umaskini yanalenga sekta ya mifugo kuongezeka kwa asilimia 9 ifikapo mwaka 2010 ili kuweza kuchangia kikamilifu katika kupunguza umasikini na kutuhakikishia usalama wa chakula. Mwaka 2010 siyo mbali, maana ni mwaka kesho kutwa tu. Ni dhahiri kwamba juhudi kubwa zaidi zinatakiwa kutoka kwenu, kwa wafugaji, wawekezaji na serikali ili kufika hapo tulipopangiwa.

Ndugu Mwenyekiti, kwa bahati nzuri Wizara imekwisha andaa Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 na inaendelea kuandaa mkakati wa kutekeleza sera hiyo. Napenda kuwahakikishia kuwa Baraza hili litashirikishwa kikamilifu katika kuandaa mkakati huo ili kwa pamoja na kwa kushirikiana na wafugaji na wadau wengine tuitekeleze Sera hiyo na malengo ya Milenia na Mkukuta kwa nguvu zetu zote.

Ndugu Mwenyekiti, mifugo mingi hapa nchini hufugwa kwa utaratibu wa mfumo wa asili wa kuhamahama Mfumo huu wa ufugaji wa kuhamahama kwa kiasi kikubwa hauna tija na ni chanzo cha uzalishaji duni wa mifugo kwa kuwa inachochea pia usambazaji wa magonjwa, uharibifu wa mazingira na kuwa chanzo cha migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi wakiwemo wakulima. Matatizo mengine ni pamoja na matumizi duni ya ardhi, uhaba wa maji na malisho, kuwepo na kuenea kwa magonjwa ya mifugo, kuwepo kwa mifugo yenye ukoosafu duni na inayofugwa katika mifumo duni ya uzalishaji, usindikaji mdogo wa mazao ya mifugo, miundo mbinu hafifu ya masoko na elimu duni ya wafugaji.

Mfumo wa ufugaji wa kibiashara kwenye mashamba ya ranchi na ufugaji wa ndani ama inavyojulikana kwa wengi *zero grazing* ni kidogo sana sawa na asilimia 3 ya mifugo yote nchini. Naomba nitumie nafasi hii kuwaomba wafugaji hao wanaohamahama watulie na kufuga kibiashara kwani hili ndilo lengo la serikali yao.

Ndugu Mwenyekiti, kwa kuwa sisi ni wadau wa sekta ndogo ya nyama, ingekuwa vema tukaitazama sekta hii kwa umakini zaidi. Takwimu za uzalishaji wa nyama zinaonyesha kuwa kumekuwepo na upungufu katika uzalishaji wa nyama kutoka tani 210,370 katika kipindi cha mwaka 2005/06 ikilinganishwa na tani 180,629 mwaka 2006/07. Sote tunafahamu kwamba upungufu huu ulisababishwa na kuwepo kwa mlipuko wa ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa ama RVF. Naamini kwamba mwaka 2007/2008 uzalishaji utapanda maana hali ni swari. Jambo jingine ambalo halifurahishi kuhusu sekta hii ndogo ya nyama ni kwamba kiwango cha ulaji wa nyama ni wastani wa kilo 10 kwa mtu kwa mwaka, ambacho ni chini ya kiwango cha kimataifa kinachopendekezwa na FAO cha kilo 50 kwa mtu kwa mwaka.

Ndugu Mwenyekiti, inawezekana sababu mojawapo ya kukua kwa kasi ndogo ya uzalishaji wa nyama ni kutokuwepo kwa chombo cha kusimamia uzalishaji wa mifugo, biashara ya mifugo na viwanda vya kusindika nyama. Upungufu huo umeifanya nchi yetu kuwa na uzalishaji mdogo na kukosa soko la uhakika la mifugo. Kumbukumbu zinaonyesha kuwa katika miaka ya hamsini na baada ya uhuru, Tanzania ilikuwa na Kampuni binafsi ya

Tanganyika Packers Limited (TPL) iliyokuwa inamiliki kiwanda cha kusindika nyama na kuendesha biashara ya nyama hapa nchini. Mwaka 1974 kiwanda hicho cha TPL kilitaifishwa kutekeleza sera ya wakati ule ya kuuweka uchumi wa nchi mikononi mwa wananchi. Kinyume na matarajio ya kuongeza tija, kiwanda hicho kilishindwa kujiendesha kwa ufanisi hivyo kupoteza cheti cha usafi (UK Sanitary Certificate) na kusitishwa kwa mkataba wa kuuza nyama kwenye kampuni ya Brooke Bond Lieberg Ltd nchini Uingereza. Bila shaka kiwanda kilipoteza sifa kutokana na usimamizi uliolegalega wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hivi karibuni biashara ya mifugo imepata msukumo kupitia jitihada mbali mbali za serikali, ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya miundombinu ya masoko hususan ujenzi na ukarabati wa minada ili kuongeza upatikanaji wa mifugo ya nyama kwa lengo la kukidhi soko la ndani na la nje. Vile vile Serikali ilijenga Machinjio ya kisasa na Chuo cha Ukataji Nyama mjini Dodoma kwa nia ya kuongeza thamani ya mifugo na nyama pamoja na kutoa elimu ya uzalishaji wa nyama. Kadhalika mwaka jana tumetoa matangazo ya kukaribisha wawekezaji binafsi kushirikiana na Serikali, kupitia Kampuni yake ya NARCO kujenga viwanda vya nyama na machinjio mapya. Nafurahi kuona kwamba wapo watanzania walioonyesha nia ya kuwekeza na mchakato wa kuanza kazi hiyo unaendelea. Pia naomba kuwapongeza wenzetu ambao tayari wameanzisha viwanda na machinjio binafsi, kwa mfano Kampuni ya SAAFI kule Sumbawanga, Kampuni ya Tanzania Pride Meat kule Morogoro na Kampuni ya Triple S ambao watawekeza kule Shinyanga. Aidha naomba

kuchukua nafasi hii kuwapongeza wafanyabiashara ya nyama ambao wameweza kuiweka Tanzania kwenye ramani ya dunia kwa nchi zinazouza na kusafirisha ng'ombe na nyama nje ya nchi. Takwimu zinaonyesha kwamba Tanzania imeweza kuuza ng'ombe 3,818 na mbuzi 606 kwenda nchi za Comoro na Burundi. Aidha, tumeuza kilo 10,701 za nyama ya ng'ombe kwenda nchi za Falme za Kiarabu na Oman na kilo 98,551 za nyama ya mbuzi na kondoo kwenda Oman, Falme za Kiarabu na Kuwait katika mwaka 2007, takwimu ambazo zinatia moyo kwa kuanzia.

Ndugu Mwenyekiti, lengo moja la kuwepo kwenu katika mkutano huu wa kwanza wa Baraza ni kufahamiana kama wajumbe wa Baraza, kupata fursa ya kuielewa Sheria ya Nyama ya mwaka 2006 ambayo imeainisha majukumu ya Baraza la Mwaka la Wadau wa Nyama ambayo ni:

1. Kuhimiza maendeleo endelevu ya Sekta ndogo ya Nyama Tanzania.
2. Kupokea na kukagua taarifa mbalimbali zitakazotolewa na Bodi ya Nyama.
3. Kupendekeza majina ya wajumbe watakaounda Bodi ya Nyama ili mimi kama Waziri mwenye dhamana ya sekta ya Mifugo niweze kuteua wajumbe wa Bodi hiyo.
4. Kunishauri na kuishauri Bodi ya nyama juu ya masuala yanayohusu kuendeleza nyama, na mambo mengine yatakayojitokeza katika utekelezaji wa Sheria ya Nyama ya mwaka 2006.
5. Kufanya kazi nyingine yoyote itakayojitokeza ili kufanikisha utekelezaji wa Sheria hii.

Ndugu Mwenyekiti, katika mkutano huu wa leo kama nilivyotangulia kusema, mtapata nafasi ya kutekeleza jukumu lenu moja kubwa la kupendekeza majina ya wajumbe watakaoteuliwa kuunda Bodi ya Nyama (The Tanzania Meat Board). Ninayo imani mtapendekeza wawakilishi wazuri wenye sifa, uzoefu na ukereketwa na Sekta ndogo ya nyama, ambao pamoja na kuisukuma mbele Sekta ya Mifugo, watanisaidia sana kuiongoza ipasavyo, maana wao watakuwa ni washauri wangu wakubwa.

Kama mtakavyokuwa mmefahamu, Bodi hii itaendeshwa na ninyi wadau hivyo ni budi kuzingatia uzoefu wenu na mazingira ya sasa ya utandawazi katika uchumi wa soko na ushindani wa kibiashara. Hivyo basi tuchague wajumbe wa Bodi wenye mtazamo wa kibiashara ambao watatuwezesha kupata masoko ya kuaminika na endelevu. Ni muhimu pia tutambue kwamba kazi ya serikali ni kuwawezesha wananchi kuanzisha vyombo vyao ambavyo vitabeba jukumu la kuendeleza sekta kwa mujibu wa sheria na kanuni mbali mbali zinazoongoza uzalishaji bora na kutafuta masoko ya mifugo, nyama na bidhaa zitokanazo na nyama.

Ndugu Mwenyekiti, narudia tena kusema kuwa maendeleo ya sekta hii ndogo ya nyama yanategemea sana hamasa ya wananchi kuingia kwenye ufugaji wa kibiashara, iwe ni watu binafsi au vikundi pamoja na juhudi zao katika kutafuta na kumiliki ardhi kwa ajili ya kupanua na kuboresha ufugaji. Aidha, naomba niwakumbushe kwamba ufugaji unaoweza kutuletea tija ni ule wa ranchi kubwa na za kati utakaotusaidia kupata mifugo bora na isiyo

na magonjwa. Ni matarajio yangu kwamba kupitia Bodi mtakayoipendekeza, vikwazo vya ufanisi katika kuendeleza soko la nyama vitapunguzwa ama vitaondolewa kabisa na hivyo kuongeza mchango wa sekta ndogo ya nyama na sekta ya mifugo kwa jumla kwenye pato la Taifa.

Ndugu Mwenyekiti, Wajumbe wa Baraza na Wageni waalikwa Baada ya kusema maneno hayo**,** naomba kuwatakia mkutano mwema wenye ufanisi na mafanikio makubwa na napenda sasa kutamka kuwa Baraza la Mwaka la Wadau wa Sekta ndogo ya Nyama **limefunguliwa rasmi.**

ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA.